**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi

*Dr. Harrison Onyango Ogutu, PhD*[1]

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100 – 20300, Nyahururu, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-7009-619X; Barua pepe ya mawasiliano: harrynamasumbi@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*30 Mei 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Propaganda, Hejemonia, Hejemonia ya Kisiasa, Hejemonia ya Kijamii, Hejemonia ya Kiuchumi, Kuhimili Hejemonia.*

**IKISIRI**

Makala hii imechunguza suala la propaganda kama mkakati wa kuhimili hejemonia katika riwaya teule za Kiswahili. Mtafiti amejadili namna propaganda inatumiwa kudumisha na kuimarisha utawala wa viongozi mintarafu ya riwaya teule. Ili kutimiza lengo lake, mtafiti amehakiki riwaya nne: Msimu wa Vipepeo, Dharau ya Ini, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi. Nadharia ya hejemonia inayoweka wazi suala la utawala wa mabwanyenye juu ya raia na kueleza udumishaji wa uwezo na mamlaka juu ya watawaliwa ni mwafaka katika utafiti huu. Mintarafu ya nadharia hii, hejemonia huendelezwa na kudumishwa sio tu kwa ushurutishaji bali pia kupitia maafikiano, lugha, wataalamu, siasa, maagizo, burudani, ujumbe na nyenzo nyingine za kielimu. Riwaya teule ziliteuliwa kimakusudi kwa kudhamiria kuwa zimesheheni masuala ya uhimili wa hejemonia. Kutokana na riwaya hizo, mtafiti alipata mitazamo mipana na tofauti ya propaganda kwa mujibu wa nguzo za nadharia na madhumuni ya utafiti. Utafiti huu ni wa maktabani ambako usomi mpana na wa kina wa riwaya teule, vitabu vya ziada, majarida na tasnifu mbalimbali ulitekelezwa. Utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo ulitumika kukusanya data huku mbinu ya kiuthamano ikitumika kuchanganua data hiyo. Muundo wa kimaelezi ulitumika kuchanganua data na kueleza matukio kwa uyakinifu. Utafiti umeonesha kuwa propaganda ni mkakati muhimu unaotumiwa na watu wenye uwezo na mamlaka kudumisha na kuhimili hejemonia katika jamii. Matokeo ya utafiti yanatoa maarifa zaidi kuhusu matumizi ya propaganda kama mkakati wa kuhimili hejemonia katika fasihi. Aidha, matokeo haya ni marejeleo muhimu kwa wahakiki na watafiti hususan wale wanaotafitia masuala ya hejemonia katika fasihi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Ogutu, H. O. (2022). Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 142-150. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686.

**CHICAGO CITATION**

Ogutu, Harrison Onyango. 2022. "Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 142-150. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686.

**HARVARD CITATION**

Ogutu, H. O. (2022) "Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 142-150. doi: 10.37284/jammk.5.1.686.

**IEEE CITATION**

H. O. Ogutu, "Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 142-150, May. 2022.

**MLA CITATION**

Ogutu, Harrison Onyango. "Propaganda Kama Mkakati wa Kuhimili Hejemonia: Mfano wa Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, May. 2022, pp. 142-150, doi:10.37284/jammk.5.1.686.

## UTANGULIZI

Mtafiti amejadili propaganda kama mkakati unaotumiwa kuhimili hejemonia mintarafu ya riwaya teule. Mtafiti amedondoa na kuchanganua data inayohusu propaganda wanazotumia wahusika walio katika nyadhifa za mamlaka kudumisha mamlaka yao. Kando na kutumia nguvu, viongozi wengi kwa werevu na ujanja, wanatumia lugha pamoja na nyenzo nyingine za kielimu kuhimili hejemonia (Gramsci, 1995). Tabaka la juu hutumia vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusu hisia na thamani zao katika jamii kwa sababu utawala hupatikana kupitia maafikiano au makubaliano (Artz na Murphy, 2000). Maridhiano na mwafaka kati ya mahejemoni na watawaliwa hata hivyo, yanaafikiwa kwa kutumia mbinu namna kwa namna ili kuwashawishi watawaliwa wakubali mawazo, dhana na itikadi za uongozi uliopo. Viongozi hususan wa kisiasa wanahimili hejemonia kwa kutumia propaganda. Wanaeneza ujumbe uliotiwa chumvi au wa uongo ili kuwashawishi raia waridhie hejemonia inayodumishwa. Kwa hivyo, hejemonia hapa inakuzwa kwa kuhusisha na kujumuisha vitendo vya kuridhisha, kudhibitisha, kuaminisha na kusadikisha raia ili wakubali matakwa ya mabwanyenye (Agnew, 2005). Mintarafu ya maoni ya Agnew, hejemonia inajumuisha vitendo vya kubembeleza, kuvuta kwa werevu, kudanganya kwa kusifusifu au kurairai wanajamii ili wafanye jambo fulani wanalolitaka mabwanyenye. Hali hii kimsingi ndio imechukuliwa kuwa propaganda katika utafiti huu.

Propaganda kwa hivyo inawasaidia mabepari na mabwanyenye kuwapumbaza raia waridhie na kuidhinisha hejemonia. Kwa kutumia propaganda, mahejemoni wanawafumba raia macho hivi kwamba raia wanaendelea kuunga mkono utawala uliopo licha ya manufaa madogo wanayopata. Mabwanyenye wanafanikisha utawala wao juu ya watawaliwa kwa kuwashawishi washirikiane na kuafikiana na mawazo ya kihejemonia (Fontana, 2008 na Gramsci, 1978). Katika hali ya kawaida, inatarajiwa kuwa raia watakosoa na kupinga unyonyaji na dhuluma zinazoendelezwa kupitia hejemonia. Hili haliwi rahisi kwa sababu asilimia kubwa ya raia wanapumbazwa kwa vishawishi anuwai kupitia propaganda. Lee (1953), anadai kuwa nia ya propaganda yaweza kuwa wazi au ya kisiri lakini lengo kuu ni kushawishi na kuathiri mitazamo, maoni na matendo ya umma. Hivyo, propaganda hapa ilitumika kushawishi raia wakubaliene na yale yanayowasilishwa pasi ya kuuliza swali lolote (Bartlett, 1940). Propaganda ilitumiwa kuwapumbaza raia wasione sababu ya kutathmini na kudadisi matendo na mitazamo ya viongozi ya waliyohimili hejemonia katika jamii.

### Msingi wa Nadharia

Nadharia ya hejemonia iliasisiwa na Antonio Gramsci, mwananadharia aliyeegemea sana

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686

mtazamo wa Kimaksi. Gramsci (1971), aliweka wazi suala la utawala na udhibiti unaoendelezwa na mabwanyenye juu ya watawaliwa. Alidai kwamba njia ya kukuza hejemonia katika jamii sio tu kutumia nguvu na kulazimisha bali pia ni kupitia maafikiano, lugha, wasomi, pamoja na nyenzo nyingine za kielimu (Gramsci, 1995). Alisisitiza kuwa tabaka la juu hutumia vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusu hisia na thamani zao katika jamii kwa sababu utawala hupatikana kupitia maafikiano au makubaliano (Artz na Murphy, 2000). Kwa hivyo, hejemonia ni hali ambapo mitazamo, desturi, thamani, itikadi na imani za watu walio katika mamlaka hutawala jamii na huaminika kuwa msingi wa hali ya kawaida ya maisha (Gramsci, 1985). Viongozi tajika wanalazimisha jamii kukubali mitazamo yao ya mambo na hali ya maisha kama hali ya kawaida. Mawazo haya yanaafikiana na maoni ya (Gramsci 1971) anaposema kuwa dhana ya hejemonia inaakisi hali ambapo kikundi kinachotawala katika jamii kinadhibiti hali na mambo katika jamii kupitia mawazo na itikadi, lakini kwa ridhaa na idhini ya watawaliwa.

Hejemonia inahusu utawala ambapo kuna mamlaka yaliyo juu ya watawaliwa.Watu walio chini ya mamlaka wanaongozwa, wanaelekezwa na kuathiriwa kwa namna moja au nyingine. Hejemonia kwa hivyo, inahusisha na kujumuisha vitendo vya kuridhisha, kudhibitisha, kuaminisha na kusadikisha mtu ili atake kile unachotaka (Agnew, 2005). Kimfumo, hejemonia inajumuisha vitendo vya kuvuta, kubembeleza, kuvuta kwa werevu, kudanganya kwa kusifusifu au kurairai wanajamii ili wafanye jambo fulani wanalolitaka mabwanyenye. Nadharia hii inahusu utawala wa kimawazo na pia utawala wa kimabavu ambapo taifa moja laweza kutawala taifa lingine kwa kutumia nguvu za kijeshi (Nella, 2017). Nella anadai kuwa siku hizi hejemonia haihusu tu matumizi ya nguvu katika uongozi bali kwa kiwango kikubwa hutegemea ushawishi wa watu wengi kwa kuwapendekezea na kuwawasilishia hali na mambo kwa njia ambayo ni vigumu sana kuyapinga au kuyakataa. Ni kwa misingi hii ambapo watu wenye nyadhifa mbalimbali katika jamii wameendelea kutumia propaganda kama njia ya kuwashawishi na kuwagagamiza raia ili waridhie utawala uliopo.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Propaganda na Hejemonia ya Kisiasa

Katika *Msururu wa Usaliti* Mheshimiwa Mbogo anapotembelea jimbo-bunge la kwake wakati wa uchaguzi, anatumia propaganda kuwaaminisha wafuasi wake kuwa ana uhusiano wa karibu sana na Rais. Mbogo anadanganya watu wa eneobunge lake kuwa kila Jumapili Rais humuita waandamane kwenda kanisani kwani huwa hana raha wasipokuwa pamoja. Maneno haya ya uongo na udanganyifu yanatumiwa na Mbogo kuwashawishi raia wakubali uongozi wake. Raia wanaamini kuwa kiongozi wao akiwa karibu na kiongozi wa taifa, maendeleo yanapatikana kwa haraka. Aghalabu wabunge kama hawa wanajipendekeza kwa Rais kama njia ya kuwafumba raia macho. Si ajabu basi kuwaona wakimwandama Rais popote aendapo na hata kutafuta mwanya wa kukaa karibu naye ilimradi waonekane. Watawaliwa wanaaminishwa kuwa uhusiano wa karibu na Rais unamaanisha raia wa eneobunge husika wanaweza kunufaika kwa kuzinduliwa miradi mbalimbali. Mawazo haya yanaafikiana na maoni ya Hummell na Huntress (1949), wanapodai kuwa propaganda huhusisha majaribio ya kuwashawishi watu wengi kwa namna yoyote ile ilimradi wakubali imani na mitazamo fulani. Hivyo, propaganda huambatana na matendo yoyote yale yanayonuia kushawishi na kuathiri imani na mielekeo ya watu. Propaganda hivyo basi inatumiwa na wabunge kama mkakati wa kuwashawishi raia waamini kuwa mbunge wao ni rafiki wa karibu wa rais na hivyo kuhimili hejemonia ya kisiasa. Raia wanaokubali kupumbazwa kwa propaganda ya namna hiyo wanasaidia kuhimili hejemonia ya kisiasa katika jamii.

Mbogo akiwa mwenyekiti wa chama cha wakulima katika *Msururu wa Usaliti*, anatumia hila kuwashawishi na kuwalaghai wakulima wenzake ili aendelee kuwatawala kiuchumi. Kwa werevu na ujanja mwingi, Mbogo anafaulu kuwashawishi wakulima kiasi kwamba wao wenyewe wanaishia kumwidhinisha kutoa shilingi milioni tano kutoka kwa akaunti ya chama ili kujenga duka na kulijaza duka hilo bidhaa. Mawazo kama vile ujenzi wa maduka ya kuuza vifaa vya ukulima kwa mikopo hayawezi kupingwa kwa urahisi hasa kwa jamii ambayo inategemea kilimo kama uti wake wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mgongo. Wanapoanza kulalamika kuhusu kutotimizwa kwa ahadi za Mbogo, mara moja Mbogo anaweka msingi wa duka kwa kutumia hela zake ili kuwanyamazisha wakulima angalau kwa muda. Katika sekta ya kilimo, wapo wakulima ambao wanaibuka kuwa mabwanyenye wanaotumia hila na udanganyifu kukuza hejemonia. Ujanja na ukora wa mabwanyenye unawapumbaza wakulima kiasi kwamba wao wenyewe wanakubali vishawishi bila ya kushurutishwa. Mawazo haya yanaafikiana na maoni ya (Gramsci, 1971) anaposema kuwa hejemonia hukuzwa na kuendelezwa kwa ridhaa na idhini ya watawaliwa. Raia wakishapumbazwa wanaruhusu bwanyenye kunufaika kutoka kwa jasho lao huku raia wenyewe wakingojea kutimizwa kwa ahadi-hewa wanazopewa kwa werevu wa mawazo. Mahejemoni kwa kuchunguza na kutathmini changamoto zinazowakumba raia, wanaibuka na mawazo yanayoonekana kuwa na manufaa kwa raia wote, hata ingawaje lengo lao la kisiri ni kujinufaisha. Maoni haya yanaoana na mawazo ya (Lee, 1953), anapodai kuwa nia ya propaganda yaweza kuwa wazi au ya kisiri lakini lengo kuu ni kushawishi na kuathiri mitazamo, maoni na matendo ya umma. Hivyo, propaganda hapa inatumika kushawishi raia wakubaliane na yale yanayowasilishwa pasi na kuuliza swali lolote (Bartlett, 1940). Propaganda inatumiwa kuwapumbaza raia wasione sababu ya kutathmini na kudadisi matendo na mitazamo ya viongozi ya wanaohimili hejemonia ya kiuchumi.

Wanasiasa mabwanyenye wanatumia hila na propaganda kuhimili hejemonia ya kisiasa kwa kufunika uovu unaotokana na utawala wao. Ripoti zote za uchunguzi kuhusu visa vya uhalifu unaotokana na uongozi zinapakwa tope kwa propaganda na hila. Kwa mfano, katika *Dharau ya Ini* waziri wa masuala ya ardhi anakuza utawala kwa hila na propaganda za kupaka tope taarifa kuhusu ripoti ya unyakuzi wa ardhi ya madongoporomoka. Anatumia uongo na propaganda kuwashawishi na kuwasadikisha raia kuwa uchunguzi wa kisa hicho na ripoti inayoandikwa inafanywa na mahasimu wa serikali. Anadai kuwa baada ya uchunguzi kufanywa, imebainika kuwa hamna ukweli wowote kuhusiana na madai yanayotolewa na gazeti la Mpapure. Waziri akiwarejelea wachunguzi wa kisa hicho anaeneza propaganda zake kwa raia kudai: "Walichofanya ni kipiga chuku, na kama mjuavyo kupiga chuku ni ukweli unaokasirisha. Na hasira ni msingi usiotegemewa kwa maamuzi!" (uk 84). Kauli hizi zinafuatiwa na kauli za viongozi wengine ambao wanashutumu vyombo vya habari kwa kukubali kutumiwa na adui wa serikali kubomoa utawala uliopo. Propaganda kwa maoni ya Lippmann (1927), Bernays (1928) na Chomsky na Herman (1988), inahusu mawasiliano na shughuli za watu walio katika nyadhifa za mamlaka na uwezo. Wanasisitiza kuwa propaganda ina chanzo chake katika serikali na mamlaka ya serikali iliyopo. Propaganda haihusu ushawishi tu bali pia anayeshawishi anafanya hivyo makusudi kwa nia ya kupitisha ujumbe kwa raia. Raia wanapumbazwa kwa propaganda na hatimaye wanaishia kuunga mkono hejemonia ya kisiasa inayokuzwa na utawala uliopo. Sababu ya viongozi wa serikali kutumia propaganda dhidi ya wakosoaji wao ni kuibua hisia za chuki miongoni mwa raia. Wanataka watawaliwa wawachukie wakosoaji na wapinzani wa hejemonia inayokuzwa. Akizungumzia hisia zinazoibuliwa na propaganda, Ross (2002), anadai kuwa propaganda huibua mwitikio wa hisia zisizofaa kama vile chuki na kiburi dhidi ya watu fulani. Hivyo, wanasiasa wanatumia propaganda kuhimili hejemonia ya kisiasa kwa kuwachochea wananchi wachukie na kubeza wakosoaji, wadhalilishaji na wapinzani wa hejemonia ya kisiasa.

Wanasiasa wanatumia propaganda kukanusha kashfa za ufisadi zinazowahusu ili kuhimili hejemonia ya kisiasa. Mawaziri katika *Dharau ya Ini* wanatumia hila na ujanja kukanusha madai ya sekta ya ardhi yaliyokuwa yamechapishwa kwenye gazeti. Kwa ujanja, hila na propaganda, wanasiasa hawa wanalalamika kuwa hizi ni njama za wakosoaji wa serikali zenye lengo la kuangusha serikali ya kidemokrasia. Wanawalaumu wapinzani wa serikali iliyochaguliwa kihalali mchana kweupe ulimwengu wote ukiona, kwa kuwapaka mawaziri wake na watumishi wake watiifu matope ya ufisadi. Kulingana nao, wao ni watumishi wa umma ambao wanatumia muda wao mwingi kama punda wa kubeba mizigo thakili ya umma. Mahejemoni wanawahadaa raia kwamba madai ya wakosoaji na wapinzani wa hejemonia iliyopo ni uongo mtupu. Wanawataka wapinzani wao watoe ushahidi ili vyombo vya sheria ya nchi vifanye kazi yake. Vyombo vya habari vinavyopeperusha ripoti za ufisadi wa uongozi vinaonywa na kutishiwa kunyang'anywa leseni zao iwapo havitakanusha madai ya uongo waliochapisha kuhusu serikali

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686

tawala. Hizi zote ni baadhi ya hila, ujanja na propaganda ambazo zinatumiwa na mawaziri serikalini kuhakikisha kuwa hejemonia ya kisiasa inadumu na kunawiri kwa idhini na ridhaa ya watawaliwa. Mintarafu ya Chomsky na Herman (1988), propaganda inatoka kwa serikali kupitia wafanyakazi wa serikali hadi kwa raia. Watawaliwa wanaosadiki hila na propaganda za viongozi serikalini wanarutubisha ukuaji wa hejemonia ya kisiasa. Hivyo, propaganda inatumiwa na mawaziri serikalini kama mkakati wa kuhimili hejemonia kwa kufunika na kuficha madhila ya hejemonia ya kisiasa.

Hejemonia ya kisiasa hukuzwa na kudumishwa kwa hila na propaganda zinazotokana na ushirikiano kati ya mawaziri wa serikali na baadhi ya watumishi wa umma. Mathalani, Waziri Mkurutu na mwanasheria mkuu Fabio Mkalla katika *Msimu wa Vipepeo* wanatumia hila kumshawishi mmiliki wa jumba la kihistoria pale Kisiwandeo ili aweze kumuuzia Adolf Dieter, mwekezaji wa kijerumani. Hali hii inathibitisha mawazo na maoni ya Bernays (1928), Lippmann (1927) na Chomsky na Herman (1988), wanapodai kuwa propaganda ina chimbuko lake katika serikali au mamlaka yaliyopo. Wafanyakazi wa serikali wanadumisha hejemonia kwa kutumia propaganda inayojumuisha hila na udanganyifu. Mathalani, Waziri Mkurutu anasema: "...lakini historia huandikwa na watu; watu kama wewe!... historia haikuzuii kuliuza... tunahimizwa kuhimiza uwekezaji ili tuinue uchumi wa nchi au labda uchumi wa huku ni bora? Unaweza kusema hiki ni kipindi cha kufuta historia..." (uk 65). Kwa hila na propaganda, Mkurutu anamlainisha mmiliki wa jumba la kihistoria hadi anaridhia mawazo anayopewa. Ikumbukwe hapa kuwa hejemonia, huwa na manufaa au faida ndogo ndogo ambazo watawaliwa hupata (Artz na Murphy, 2000). Kwa kiwango fulani, hejemonia huwafaidi hata wanyonge katika jamii ila kwa kiwango kidogo sana. Manufaa haya yanawafumba macho raia kiasi cha kutoona ubaya na uozo wa viongozi wanaohimili hejemonia ya kisiasa. Mahejemoni wanatumia udanganyifu na propaganda kuhakikisha kuwa watawaliwa hawaoni asilimia kubwa ya manufaa yanayoishia mifukoni mwao. Propaganda kwa hivyo inakuwa mkakati unaotumiwa kuhimili hejemonia ya kisiasa kwa kuwapumbaza raia wasione manufaa wanayopata wanasiasa.

Viongozi wa kisiasa wanahimili hejemonia ya kisiasa kwa kutumia propaganda kuficha siri za dhamira yao katika uongozi na utawala. Akizungumzia suala la hadaa na hila za kisirisiri kama propaganda Lee (1953), anadai kuwa propaganda inaweza kudhihirika kisiri kwa nia ya kushawishi na kuathiri mitazamo, maoni na matendo ya watu. Mathalani, maelezo anayoyasoma Waziri Mkurutu katika kitabu kinachozungumzia hadaa, kuna mmea uitwao *Dionaea muscipula* ambao hutoa ua la uongo kuwavutia wadudu ambao wanapolifikia wanamezwa na kuishia kuwa mlo. Hivi ndivyo viongozi wa kisiasa wanavyotumia uongo na hila kuwahadaa raia kwa nia ya kutaka kufaidika wenyewe huku raia wakiumia na hata kuangamia. Mkurutu anaamini kuwa iwapo virusi hutumia ujanja kuweza kuishi katika mwili wa binadamu, sharti binadamu naye atumie ujanja ili kuweza kuishi katika ulimwengu huu wenye changamoto tumbi nzima. Kinachobainika hapa ni kuwa ukuaji na udumishwaji wa hejemonia unategemea uwezo wa viongozi kutumia hila na propaganda. Mahejemoni wa kisiasa wanatumia propaganda kuchezea akili za raia na kuwasababisha waridhie na kuidhinisha hejemonia ya kisiasa. Kwa kukosa kutambua hadaa na propaganda za viongozi na kuziepuka, maisha ya raia yanadhurika. Raia wanyonge wanaishia kugandamizwa kwa propaganda na udanganyifu wa mahejemoni wanaohimili hejemonia ya kisiasa.

Viongozi wa kisiasa katika *Msimu wa Vipepeo* wanawahadaa raia kwa kulia machozi mbele ya hadhira wanapojitetea kuhusiana na sakata zinazowakabili. Waziri Mkurutu anapukutikwa na machozi ili kuwasadikisha raia kuwa hana hatia yoyote kuhusiana na madai ya kuhusika kwake katika kashfa za ufisadi. Kwa mujibu wa Mkurutu mwenyewe, machozi yana uwezo mkubwa sana hasa ukijua wakati wa kuyatoa. Machozi yana uwezo wa kusema jambo ambalo lugha ya kawaida hushindwa kusema, (uk. 100). Waziri Mkurutu anatokwa na machozi anapotetea sakata chafu inayomwandama kwa manufaa yake mwenyewe. Wanasiasa wanatumia hadaa ya machozi kujinasibisha na raia wanaowaonea huruma wanaposhambuliwa na kukosolea na wapinzani. Kwa kufahamu namna kulia machozi kunavyogusa hisia za watu, wanasiasa wanatumia sanaa ya machozi kuwapumbaza na kuwashawishi waridhie na kuidhinisha hejemonia ya kisiasa. Maoni haya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

yanaafikiana na mawazo ya (Ross, 2002), anapodai kuwa propaganda huambatanishwa na hila, udanganyifu na ushawishi wa kuchezea saikolojia ya watu ili kuvuta hisia zao. Katika hali hii fikra na mawazo ya watu yanazugwa kiasi cha kutofanya maamuzi ya kibinafsi. Hivyo, kulia machozi mbele ya wananchi wanaohutubiwa ni propaganda inayotumiwa na wanasiasa ili kuhimili hejemonia ya kisiasa. Raia wanaosadiki propaganda za viongozi wa kisiasa wananawirisha uongozi wa kihejemonia kwa kukosa ujasiri wa kuukabili, kuukosoa na kuupinga.

Kwa kufahamu kuwa michemko ya hisia za kulaumu, kulaani, kukashifu, kutusi na kuikosea serikali adabu hutibuliwa na sakata mbalimbali zinazowahusisha wanasiasa, propaganda zilitumiwa kuwatuliza raia. Kwa mfano, katika *Msimu wa Vipepeo* wakazi wa Kisiwandeo kwa kupumbazwa na hila za waziri Mkurutu, wanaishia kudai kuwa hawakuwa wametengwa kama walivyofikiria hapo awali. Waziri Mkurutu anasema kuwa hisia za umma ni kama povu ambalo huongezeka na kuvimbiana lakini likipulizwa baada ya muda huyeyuka na kupotea kabisa na hatimaye hali ya awali hurudi. Ni kwa misingi hii ndipo kunapotokea kashfa ya mauaji ya Yusuf Idris. Mkurutu anawahadaa wananchi kwa ushauri anaoutoa. Waziri Mkurutu anashauri kwamba polisi wamkamate Gattuso Berlusconi (mwandani wake), watoe matamshi makali dhidi yake na kisha kumfungulia mashtaka kama njia ya kuzima kelele zilizoko. Polisi nao kwa kuheshimu mamlaka ya dola, wanatekeleza ushauri huo na kutangaza kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria na kwamba watahakikisha kuwa wameinua mawe yote katika uchunguzi wao. Raia kwa kupumbazwa na propaganda hizi za Mkurutu wanahongera uamuzi wa serikali; uamuzi ambao unapeperushwa kwa vyombo vya habari huku raia wanasherekea na kushangilia. Baada ya siku chache Guttuso Berlusconi anaachiliwa huru. Hivyo, mawaziri serikalini wanatumia propaganda kuhimili hejemonia ya kisiasa na kiuchumi kwa kuwalinda na kuwatetea wendani wao ambao huhusika katika visa vya uhalifu. Propaganda zinaenezwa kupitia vyombo vya habari ili idadi kubwa ya raia ifikiwe na kushawishiwa kuunga mkono uamuzi wa serikali tawala. Propaganda zinatumiwa kuhimili hejemonia ya kisiasa kwa kufunika uovu unaotendwa na mahejemoni.

Kisa cha mauaji ya Yusuf Idris katika *Msimu wa Vipepeo* kilifaa kusababisha malalamishi na kilio cha haki kutoka kwa wakazi wa Kisiwandeo. Licha ya udhalimu huo, wakazi hao wanafumbwa macho na propaganda na kuishia kuridhia hejemonia ya kisiasa inayokuzwa na kudumishwa na viongozi wa kisiasa. Viongozi wa kisiasa katika serikali wanatumia propaganda kuwatuliza raia wanaoghadhabishwa na ukatili wa wawekezaji. Wanachezea hisia za raia kwa kuwapumbaza na vitendo vinavyoashiria uwajibikaji ilhali ni uzandiki mtupu. Ukweli ni kwamba lengo la wanasiasa hawa ni kupata idhini na ridhaa ya kuendeleza hejemonia ya kisiasa na kiuchumi. Kwa mujibu wa (Ross, 2002), propaganda inaenezwa na asasi fulani ya kisiasa kwa mpangilio na sababu fulani. Kwa hivyo propaganda inatumiwa kama mkakati wa kuhimili hejemonia ya kisiasa kwa kuwahadaa wananchi kuwa serikali inajali usalama wao. Kwa njia hiyo, hejemonia ya kisiasa inahimiliwa, inakua na kuendelea kunawiri.

**Propaganda na Hejemonia ya Kijamii**

Wanandoa pia wanatumia propaganda kuwahadaa wenzao ili kuwatawala kimawazo. Wanaume wanawatawala wanawake katika ndoa kwa kutumia mbinu za kijanja ilimradi wapate chochote wanachokitaka. Kwa mfano, Mzee Magu katika *Msururu wa Usaliti* anamhadaa mkewe (Naito) kwa kujifanya kuwa mzuri. Baada ya kutambua kuwa tabia yake ya ulevi wa kupindukia na kutowajibika pale nyumbani imemfanya mkewe kumpuuza na kutomhusisha katika mipango yote muhimu, anabuni mbinu ya kuweza kumhadaa na kumshawishi ili aridhie kumpa habari anazotaka. Magu anarauka mapema kukata majani ya kumlisha ng’ombe wakati wa kukama, anayatia kwenye hori, anayakatakata na kumwachilia ndama kisha anaandaa ng’ombe tayari kukamwa. Zaidi, Magu anapasua gogo la mti ili kupata kuni. Siku hiyo hata chamcha anakula nyumbani. Hii ni kazi ambayo Magu hajaifanya kwa miaka mingi sana tangu amwoe Naito. Kwa njia hii, Magu anampumbaza mkewe na kuyeyusha moyo wake kiasi cha kumsababisha aridhie kumpa habari ambazo alikuwa amekula yamini kutompa. Wanaume wanatumia hila katika ndoa zao kudumisha hejemonia ya kiume juu wake zao. Wakitafuta ridhaa ya wake zao, wanaume wanatumia propaganda kuwabembeleza ilimradi wafaulishe

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686

utawala wao katika ndoa. Hali hii inathibitishwa na mawazo ya Bartlett (1940), anayedai kuwa propaganda inalenga kuathiri na kushawishi mawazo na tabia za hadhira kwa namna kwamba hadhira hufanya yote wanayoshawishiwa kufanya bila kutaka kujua sababu za kufanya hivyo. Wanawake wasiokuwa na uwezo wa kutambua hila za wanaume wanaishia kuridhia hejemonia ya kijamii inayokuzwa na wanaume katika ndoa. Hivyo, propaganda ni mkakati unaotumiwa na wanaume kukuza na kudumisha hejemonia ya kijamii katika asasi ya ndoa.

Aidha, katika *Msimu wa Vipepeo* Waziri Mkurutu anahimili hejemonia ya kijamii kwa kutumia hila na propaganda. Kwa kutambua kwamba binti yake (Ndumi) amejua mengi kumhusu hususan tangu ile siku alipomsikia akizungumza kwa simu na mpenzi wake wa pembeni, Mkurutu anatumia ujanja na hila kumfumba Ndumi macho ili asije akatoboa siri; siri ambayo ingeharibu uhusiano wake na mkewe Julia. Mkurutu kwa ujanja na hila nyingi anafanya juhudi za kuonyesha upendo kwa Ndumi, hali ambayo haijakuwepo kwa muda mrefu. Mathalani, sasa anaweza kupata wasaa wa kuandamana na bintiye na kwenda kununua vitabu, kwenye sherehe za kuzaliwa za marafiki zake na hata kufuatilia maendeleo yake ya kucheza piano. Hali hii ni ya kawaida katika ndoa nyingi zinazoongozwa kihejemonia. Wanandoa, hususan wanaume wanatumia ujanja na hila kuwahadaa wenzao wa ndoa ili kufunika madhila ya uongozi wao. Zawadi za hapa na pale kwa watoto ni kama chambo cha kuwavuta karibu na kuwashawishi kwa kuwapumbaza watoto waridhie hejemonia ya kijamii. Matumizi ya takrima kwa watoto na hata wanandoa wenza ni hila na hadaa ya kuyeyusha mioyo ya wapokezi wa tunu zenyewe ili wasikosoe hejemonia ya kiume inayokuzwa. Wanaume wanatumia propaganda kufunika uovu wao ili kuhimili hejemonia ya kiume katika ndoa na familia kwa jumla.

Hejemonia imekuzwa na kudumishwa kwa kutumia propaganda, hila na ujanja katika *Dharau ya Ini*. Mathalani, mamake Deborah anamweleza Deborah jinsi watu wananyang'anywa ardhi zao na Kivu, kwa kutumia cheo chake kama chifu wa eneo hilo. "Huyo Kivu - sitamsahau hata katika ufu wangu – alitumia ujanja kuwanyang'anya watu mashamba yao" (uk. 260). Kila mara watu wanapolalamika, Kivu anaita mwapiza kiapo kuamua ukweli huo. Jamii hii inaamini kiapo kuliko vyombo vya sheria. Wanaenda kwenye ardhi inayogombaniwa ili kula kiapo. Kila mara Kivu anaapizwa akiwa amevaa viatu. Inabainika baadaye kuwa kila mara Kivu anapoenda kuapishwa, anachota mchanga kutoka kwenye ardhi yake halali na kuweka kwenye viatu vyake na ndio anaousimamia akiapa. Mabwanyenye wanatumia ujanja, hadaa na mizungu ya ushirikina kupata idhini ya watawaliwa kukuza hejemonia ya kiuchumi katika jamii. Imani za watawaliwa kwa mambo ya kishirikina kama vile kula viapo zinawapa mahejemoni mianya ambayo inatumiwa kwa werevu kupata kibali cha kudumisha hejemonia ya kiuchumi. Kwa kuzingatia imani za kishirikana katika jamii, mahejemoni wanatumia hila na propaganda kuhakikisha kuwa hejemonia ya kiuchumi inanawiri bila ya upinzani.

Matumizi ya hila na propaganda kudumisha hejemonia pia yanadhihirika katika *Majilio ya Mkombozi* kupitia visa viwili. Kisa cha kwanza ni mashindano ya kupiganisha mafahali ambapo mintarafu ya utamaduni washiriki ni watoto wavulana pekee. Ilonkundemi anayeleta fahali wa mjomba wake. Anatumia njia ya udanganyifu ili apate ushindi. Ilonkundemi anatumia uganga ambapo anamnong'onezea fahali wake maneno fulani kisha akampaka kitu fulani mdomoni. Mwamuzi mkuu na watu waliopo wanashangaa kwani kitendo hicho kinaonekana kama mazingaombwe. Hata hivyo, Ilonkundemi anatangazwa kuwa mshindi hata kama uamuzi huo si haki. Ilonkundemi na mjombake Wapukorengonyi wanapata ushindi na kutuzwa kwa kutumia hila na udanganyifu.

Kisa cha pili ni pale ambapo Wapukorengonyi anatamani mpwa wake (Ilonkundemi) awe mwana wa Miwambo, yaani mkombozi wa jimbo la Miwambo katika Majilio ya Mkombozi. Hakuna anayejua dalili au sifa zozote kuhusu mwana wa Miwambo isipokuwa Musemangikweli ambaye hajamweleza yeyote juu ya dalili hizo. Wapukorengonyi kwa hila zake anapanga na kubuni dalili hizo na kuzitia katika mwili wa Ilonkundemi. Anajua kwamba kwa sababu Musemangikweli ni kipofu, hana uwezo kuziona na kuzitambua dalili hizo, kwa hivyo mtu kuzibuni na kusema ndizo, zitakuwa ndizo (uk. 95). Hizi ni hila na hadaa wanazotumia mabwanyenye kukuza na kudumisha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686

hejemonia ya kiuchumi katika jamii. Wanawahadaa raia kwa kuamini kwamba baadhi ya viongozi katika jamii ni vipofu wasioweza kutambua na kushauri jamii kuhusu sifa za kiongozi bora.

Hivyo, katika *Majilio ya Mkombozi* suala la uongozi na hejemonia linaelezwa kwa njia ya mafumbo na taashira. Mashindano ya wafugaji bora ya kuwapiganisha mafahali ni taashira ya siasa na uongozi unaoendelezwa kihejemonia. Kwanza, kuna jamii ambazo zinaridhia hila na uongo kwamba siasa na uongozi wa jamii ni shughuli ya wanaume pekee. Katika jamii kama hizi, vijana wavulana wanaandaliwa mapema kurithi nafasi za uongozi kutoka kwa watu wa ukoo zao hususan katika familia ili kudumisha hejemonia. Hivyo, wavulana wanazoeshwa majukumu ya uongozi mapema kwa kuaminishwa kuwa uongozi wa jamii ni jukumu la wanaume pekee. Wanawake wanaachwa nje ya vinyang'anyiro vya uongozi wa jamii na kupewa majukumu mengine yasiyohusiana na uongozi. Hali hii inawafinyanga wavulana na kuwafanya mababedume wanaowatawala wanawake katika familia hususan katika ndoa wakishakomaa.

Pili, kinyang'anyiro cha kutafuta na kudumisha ubabe wa kisiasa na uongozi kimejaa hila, udanganyifu na propaganda. Haya yanadhihirika kupitia juhudi anazofanya Wapukorengonyi ili kumpa Ilonkundemi sifa za Mwana wa Miwambo katika *Majilio ya Mkombozi*. Mabepari wako tayari kufanya chochote cha haki au haramu kuhakikisha kuwa hejemonia inadumishwa. Mahejemoni wanatumia kila mbinu ya udanganyifu kushawishi watawaliwa waidhinishe utawala uliopo kwa kuunga mkono maamuzi yote yanayofanywa. Viongozi hawa wanaochaguliwa na kuidhinishwa na raia wanaishia kuwa mahejemoni wanaoipumbaza jamii kwa hila chungu nzima huku jamii hiyo ikiendelea kugandamizwa. Hila na propaganda ni mkakati unaotumiwa na wanasiasa kwa nia ya kushawishi watu wengi ili wakubaliane na mawazo yanayowasilishwa (Ross, 2002). Hivyo, hejemonia ya kisiasa inahimiliwa kwa matumizi ya propaganda na hila zinazowezesha ushawishi na udhibiti wa mawazo ya watawaliwa.

**Propaganda na Hejemonia ya Kiuchumi**

Sekta ya ajira inashuhudia uimarishaji wa hejemonia ya kiuchumi. Baadhi ya waajiri ni mabwanyenye wanaoendeleza na kudumisha utawala kwa kutumia ahadi za uongo na hila ili kuwapa matumaini waajiriwa. Musa katika *Msururu wa Usaliti* anamtahadharisha Sera kuhusu wema na ukarimu wa mwajiri wake. Akimuonya Serah, Musa anasema: "Lakini tahadhari usiwaamini sana watu wa mjini. Wana ujanja mwingi. Anaweza kukupa matumaini ya bure ili uendelee kumtumikia." ( uk. 123). Baadhi ya waajiri wanatumia ujanja na hadaa kuwapa waajiriwa matumaini ya uongo. Kwa hila na udanganyifu, waajiri wanawapumbaza na kuwaaminisha waajiriwa kwamba maslahi yao yanashughulikiwa kikamilifu. Kwa njia hii, waajiriwa wanatawaliwa kimawazo kama njia ya kuwafanya waendelee kufanya kazi bila ya kukosoa wala kuasi dhidi ya hejemonia inayokuzwa na waajiri. Katika hali kama hii, waajiriwa wanalipwa mishahara midogo, marupurupu ya hapa na pale na vyumba uchwara vya makazi kama mtego wa kuwanasa waidhinishe hali ilivyo. Hizi faida ndogo ndogo wanazopata waajiriwa zinawafumba macho baadhi yao wasione ukweli kwamba hejemonia inayokuzwa ni gandamizi na hatari kwa maisha yao. Maoni ya Hummell na Huntress (1949), kwamba matendo yoyote yale yanayonuia kushawishi na kuathiri msimamo wa watu ni propaganda yanashadidiwa na mawazo haya. Hivyo, propaganda inatumiwa kuhimili hejemonia ya kiuchumi kwa kuwapa raia matumaini ya maisha bora kupitia ahadi za uongo na zawadi za hapa na pale.

## HITIMISHO

Imebainika wazi kuwa katika *Msururu wa Usaliti*, *Majilio ya Mkombozi*, *Dharau ya Ini* na *Msimu wa Vipepeo*, viongozi wanafanikiwa kukuza na kuendeleza hejemonia ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa kutumia Propaganda. Propaganda inayotumiwa inalenga kuwapumbaza na kuwashawishi watawaliwa ili waridhie na kuidhinisha hejemonia inayohimiliwa pasi na kukosoa mawazo yanayokuzwa na viongozi. Hata hivyo, propaganda inafaulu tu pale ambapo raia wenyewe wanaridhia na kuidhinisha uwepo wa hejemonia husika katika jamii. Mawazo haya yamepigwa jeki na maoni ya (Fontana, 2008) na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.686

(Gramsci, 1978) wanaposhikilia kuwa ushirikiano mwafaka na makubaliano kati ya watawala na watawaliwa ni msingi wa kunawiri na kufaulu kwa hejemonia katika jamii. Kwa hivyo, kuwepo kwa hejemonia katika jamii kunatokana na ridhaa na idhini ya raia wanaotawaliwa; raia wanaoridhia ushawishi katika propaganda inayotumiwa na viongozi tawala.

## MAREJELEO


Agnew, J. (2005). *Hegemony: The New Shape Of Global Power*. PHILADELPHIA: Temple University Press. http://www.jstor.org/stable/j.ctt14bsxmk

Artz, L., & Murphy, B. O. (2000) *Cultural Hegemony in the United States*. California: Sage Publications.

Bartlett, F. C. (1940) *The aims of Political Propaganda.* Octagon: New York.

Bernays, E. (1928) *Propaganda.* New York: Liveright.

Chomsky, N., & Herman, E. (1988) *Manufacturing Consent: The Political Economy of the Mass Media.* New York: Pantheon.

Fontana, B. (2008) *'Hegemony and Power in Gramsci' in Howson, R. and Smith, K. (eds), Hegemony: Studies in Consensus and Coercion*, Routledge, New York.

Gramsci, A. (1995) *Further selections from the prison Notebooks.* Edited and translated by Derek Boothman. Minneapolis: University of Minnesota press.

Gramsci, A. (1978) *Selections from the Political writings 1921-1926*, Lawrence and Wishart, London.

Gramsci, A. (1971) *Selections from the prison Notebooks.* Q. Hoare and G.N. Smith, eds and trans. London. Lawrence and Wishart.

Hummell, W. &, Huntress K. (1949) *The Analysis of Propaganda*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Lee, A. (1953) *How to Understand Propaganda.* New York: Rinehart.

Lippmann, W. (1927) *The Phantom Public*. New York: Macmillan.

Nella, P. (2017) *The Many Faces of Power:* The Portrayal of Hegemony in *Fight Club* by Chuck Palahniuk and *American Psycho* by Bret Easton Ellis. University of Tamperes Press.

Ross, S. T. (2002) *Understanding Propaganda: The Epistemic Merit Model And its Application to Art.* The Journal of Aesthetic Education. Spring 2002, Vol 36. No 1 pp. 16-30. University of Illinois Press.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.